KIGOMA DISTRICT COUNCIL
P. O. Box 332

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA.**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA.

Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma inapenda kuwatangazia wananchi wote kwamba,Serikali itauza kwa njia ya Mnada wa Hadhara Magari,Pikipiki,Mitambo na Vifaa mbalimbali chakavu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma majengo ya zamani yaliyopo Kigoma mjini barabara ya Kuelekea Ofisi za Madini.

Mnada huu unatarajiwa kufanyika siku ya **Alhamisi ya tarehe 29.05.2025** kuanzia **saa 4:00 asubuhi** .hivyo wananchi wote mnakaribishwa.

### MASHARITI YA MNADA.

1. Chombo/kifaa kitauzwa kama kilivyo mahali kilipo;
2. Mnunuzi atalazimika kulipa hapo kwa papo amana (depositi) isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya chombo/kifaa alichoinunua,na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada.Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa chombo/kifaa husika na amana iliyolipwa haitarudishwa:
3. Mnunuzi atawajibika kulipia kodi zote stahiki kwa mujibu wa Sheria.
4. Mnunuzi atatakiwa kuondoa/kuchukua chombo alichonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
5. Ruhusa ya kuangalia vyombo/Vifaa itatolewa siku mbili (2) kabla ya mnada husika.

**MKURUGENZI MTENDAJI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA.**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KIGOMA

CamScanner